

**SHULE YA UPILI YA KIPSUTER**

**MTIHANI I MUHULA II, 2017**

**KIDATO CHA KWANZA**

**KISWAHILI**

Jina: \_\_\_\_\_ Nambari: \_\_\_\_\_ Darasa: \_\_\_\_\_ Tarehe: \_\_\_\_\_

**Maagizo:**

i). *Hakikisha kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

ii). *Jibu Maswali yote kwenye nafasi ulizoachiwa.*

**1. Sauti hizi ni za aina gani? (alama 1)**

a) /l/ (alama 1)

b) /h/ (alama 1)

**2. a) Eleza maana ya sauti ghuna. (alama 1)**

b) Toa mfano wa sauti ghuna inayotamkwa menoni. (alama 1)

**3. Tenganisha kitenzi kifuatacho katika viambishi vyake na uonyeshe maana zao za kisarufi.**

(alama 3)

Ulimpikia

4. Weka shadda kwenye maneno yafuatayo:

a) Mchwa. (alama 1)

b) Mteremko. (alama 1)

5. Andika sentensi zifuatazo ziwe katika hali au nyakati zilizowekwa mabanoni.

a) Maria anapenda kulia kwa sauti. (*mazoea*) (alama 1)

b) Zuhura atawakaribisha wageni wake. (*wakati uliopo*) (alama 1)

6. Tunga sentensi yenye aina zifuatazo za maneno.

N+V+T+E (alama 2)

7. Sahihisha:

Vitabu zangu imeibwa yote. (alama 1)

8. Kwa kutolea mfano wa sentensi, eleza matumizi moja ya alama ya kipumuo. (alama 2)

9. Weka nomino hizi katika ngeli zao:

a) Majeruhi (alama 1)

b) Mto (alama 1)

**10.** Kanusha sentensi zifuatazo:

a) Wewe ulipigia darasa letu. (alama 1)

b) Mkulima akipalilia mahindi yake, atapata mavuno mengi. (alama 1)

**11.** Vipashio vya lugha ni nini? (alama 1)

**12.** Eleza miundo miwili ya nomino katika ngeli ya KI-VI na utoe mifano ya nomino katika kila miundo. (alama 2)

**13.** Ainisha silabi katika maneno yafuatayo:

a) Pweza. (alama 1)

b) Lugha(alama 1)

**14.** Akifisha sentensi zifuatazo:

a) kikoi hiki kilikuwa changu lakini nilimwachia rafiki yangu. (alama 2)

b) ukulima hutegemea mambo mengi hali ya anga ndiyo muhimu zaidi. (alama 2)

**15.** Taja aina ya sentensi ifuatayo ukizingatia kupanda au kushuka kwa sauti inaposomwa.

Yeye ni mwerevu! (alama 1)